

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS –TAMISEMI

KAZI YA NYUMBANI KIDATO CHA PILI APRILI 2020

NAMBA: 021

KISWAHILI

MUDA: SAA 2: 30

MAAGIZO

- Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E
- Jibu maswali yote.

KWA MATUMIZI YA WATAHINI TU

NAMBA YA SWALI	ALAMA	SAINI
01		
02		
03		
04		
05		
TOTAL		

SEHEMU A: (ALAMA 15)

UFAHAMU:

1. Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata:-

Dalali alianza kumnadi beberu akisema” Haya leo tena jamani sogeeni mjipatie vitu bei nafuu. Oneni mnyama mnono huyu, shilingi elfu sita na mia tano. Nani atakaye na atalipa ngapi? Mzabuni wa kwanza alipandisha bei hadi shilingi elfu saba na mia mbili. Toka hapo bei ilizidi kupanda vikali ajabu, hatimaye mzabuni wa mwisho alikubali kutoa elfu kumi.

MASWALI

- (a) Dalali alitaja bei gani kama kianzia cha bei ya Beberu.
- (b) Mzabuni wa kwanza alitaka kulipa shilingi ngapi?
- (c) Eleza“ haya tena Jamani Sogeeni” ina maana gani?
- (d) Eleza maana ya maneno yafuatayo:-
 - (i) Dalali
 - (ii) Zabuni
 - (iii) Nafuu
- (e) Andikakichwa cha habarihi.

SEHEMU B: (ALAMA 15)

UTUMIZI WA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

2. (a) andika tungo zifuatazo kwa usahihi:-
 - (i) Juma ni mwizi. Ameniiba fedha zangu Usahihi.....
 - (ii) Ninachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kumaliza kidato cha pili. Usahihi.....
 - (iii) Siku wanajua mwalimu wa Kiswahili anaitwa Huba Usahihi.....
 - (iv) Katika ajali hiyo watu kumi waliuawa. Usahihi.....

- (v) Ng'ombe zangu zimeibiwa.
Usahihi.....
.....
- (b) Andika rejesta ya kila sentensi kulingana na muktadha wake.
- i) Ndiyo afande ! nitawapeleka sasa hivi
.....
 - ii) Tumia moja kutwa mara tatu
.....
 - iii) Kituo kinachofuata ni mkuhungu nani anashuka?
.....
 - iv) Chirwa alimpiga chenga bocco, hatimae akaipatia yanga goli.....
 - v) Ndege nyingi zilikuwa zikitua na kupaa
.....
- c) Oanisha orodha A na B kujenga dhana sahihi

ORODHA A	ORODHA B
(i) Muktadha	A. Mazingira ya jambo husika .
(ii) Fanani	B. Lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi.
(iii) Niaje? Mishe, kimenuka	C. Ni mtindo wa lugha inaozungumzwa kulingana na muktadha na kusudi maalumu.
(iv) Rejesta	D. Manju/ mtambaji wa kazi za fasihi
(v) Tanzuzalugha.	E. Baadhi ya misimu.

SEHEMU C ALAMA 15

SARUFI I:

3. (a) Andika aina ya neno lililopigiwa mstari.
- (i) Mtoto mchanga ameumia.
 - (ii) Nitakwenda shuleni
 - (iii) Nani amefika?
 - (iv) Ameondoka leo
 - (v) Wewe umpole
- (b) Onesha kazi ya viambishi awali katika maneno yaliyopigiwa mistari

- Mfano:** leo sijala chochote.
“si” kiambishi awali kinachoonesha ukarusha.
- (a) Amina na Asha wamebadilishana nguo
 - (b) Mbona mlichelewa kufika kazini.
 - (c) Mwalimu aliyefika anafundisha
 - (d) Mimi nitashinda mbio hizi
 - (e) Mwanafunzi anasoma kitabu
 - (f) Tunga sentensi kwa kutumia vipashia vifuatavyo:-
 - (i) W + t + N
 - (ii) N+ V + Ts + T + E
 - (iii) N + T + N
 - (iv) W + TS TS + T + E
 - (v) T

SEHEMU D (ALAMA 40)

FASIHI SIMULIZI

4. (a) Eleza dhima nne (4) za fasihi kwa jamii.
(b) Eleza maana ya istilahii zifuatazo:-
- (i) Vina (ii) Hadhira (iii) Fani (iv) Mizani (v) Dhamira
- (c) Fasihi simulizi hujitokeza katika tanzu kuu nne.
Taja tanzu hizo na kwa kila tanzu taja vipera viwili:-

TANZU	VIPERA
(I)	(i)
(II)	(ii)
(III)	(iii)
(IV)	(iv)

- SEHEMU E (ALAMA 15)**
- #### **UANDISHI WA INSHA / UTUNGAJI**
5. Wewe kama kiongozi wa mazingira, andika barua kwa mkuu wa shule umuombe vifaa vya usafi.
Barua hiyo ipitie kwa mwalimu wa mazingira, shule yako ni shule ya sekondari JUHUDI S.L.P 712 KONDOA.